

Kanuni takatifu iliandikwa na Mchungaji Sun Myung Moon huko Korea. Ujumbe wake ulioandikwa kwa lugha ya Kikorea ulitafsiriwa kwa mara ya kwanza kwa Kiingereza na sasa umetafsiriwa kutoka Kiingereza hadi Kiswahili. Kanuni hii takatifu inafungua njia kwa yule anayetafuta majibu ya ukweli kwa maswali mengi ya kimsingi hii si tafsiri rasmi kwa mujibu wa baraza la Kiswahili Bakita na tunaomba kwa unyenyekevu msomaji asiwe mkali hata kidogo katika uwasilishaji na tafsiri, jambo ambalo si la moja kwa moja. kutoka Makao Makuu ya kanisa la umoja, lakini kwa wafuasi rahisi na wa kujitolea wa Baba Moon, wanapotaka kusambaza ujumbe wake kwa watu wanaozungumza Kiswahili. Tunapenda kukualika usome kwa makini kitabu hiki kitakachokupa maono mapya ya ulimwengu. na itabadilisha maisha yako yote.

# UKOMBOZI NA BARAKA

**(Restoration and blessing)**

Hotuba iliyotolewa february 12,1969.
Tokyo Japan

---

.

Hakuna mtu hata mmoja aliyeelewa ya kwamba historia ya binadamu ilikuwa historia ya ukombozi. Fanikio kubwa la Kanisa la Umoja ilikuwa kuona matukio yote ya kihistoria kuwa ni utaratibu wa ukombozi. Mungu ndiye asili ya msingi huo wa kihistoria. Yeye alikuwa mwendeshaji wa historia yote hadi siku za hivi karibuni na kuifanya historia yote kuendelea. Kwa sababu ya kusudi lake Mungu, kila mtu, familia, makabila pia mataifa walipewa majukumu ya ukombozi, na kwa kupitia wao wote, historia iliendelezwa hatua kwa hatua. Hivyo, hoja kuu ya historia inapaswa kuwa, historia hii ya ukombozi itakamilika lini? Kusudi la ukombozi litakamilika lini?

Kumalizika kwa ukombozi ina maana kwamba ukombozi katika viwango visivyokamilika, kwa mfano: kiwango ambacho hakikukamilishwa na Adam kwa sababu ya kuanguka kwake, pia kiwango ambacho hakikukamilishwa na Yesu. Haya yote yanahitaji kurudishwa kwa kulipia malipizi. Hii ndiyo kazi ya Kanisa la Umoja. Naongoza njia na waumini wote Duniani wa Kanisa la Umoja wanapaswa kuifuata. Ni wajibu wangu kuwaacha waumini wote wanaoshughulika kuvikomboa viwango hivyo vyote ambavyo havikumalizika. Ni wajibu wenu kufanya hivyo kulingana na mwongozo wangu.

Mwanaume ambaye anayo kazi muhimu kama hii angehitaji kuwa mkubwa kuliko Adam, pia kukamilisha lengo kwa niaba ya Yesu. Mwanamke ambaye anashirikiana na mwanaume huyo angehitaji kumzidi Hawa pia kukubalika kuwa mke mpya wa

Yesu. Utume wa Kanisa la Muunganisho ni kuzaa mwanaume pia mwanamke kama huyo.

Yesu alisulubiwa. Kwa sababu hiyo, msingi wote wa kidunia ulipotezwa. Kile ambacho Yesu hakukimaliza kingehitaji kulipiwa na kila mmoja wetu. Kwa njia hii, kila mmoja wetu angehitaji kumzidi Yesu.

**Njia ya Kupingwa:**
Ili kutuwezesha kukomboa yale yote yaliyopotea, inatupasa kutimiliza upeo maalum Duniani kwa kupitia mapingamizi yote ya kihistoria. Kwa sababu hii, inatupasa kudhulumiwa na watu wote, na hatimaye tunapaswa kuwashinda wote. Bila njia ya mateso ya aina hii, ukombozi kwa njia ya malipizi hauwezi kukamilika.

Hata hivyo hii ilikuwa njia ya Kanisa la Muunganisho. Ilikuwa kila wakati vigumu na kunyanyaswa, lakini halikujitetea kamwe. Tulikuwa tunanyanyaswa na viwango vya mtu mmoja, familia, kabila na taifa, na tulijikuta katika ukiwa wakuzidi. Tena ilitupasa kumtuliza Mungu katika hali ya aina hiyo. Hii ilikuwa historia nzima ya Kanisa la Muunganisho. Inabidi mjue haya yote. Hakuna hata mmoja anayeelewa, ni mimi peke yangu ndiye ninafahamu kabisa.

Yesu alipingwa hata na wafuasi wake wakuu watatu. Wafuasi watatu ni ishara na uwakilisho wa mataifa matatu Duniani. Kwa hivyo, hapo tulipovumbua njia yetu na kiwango cha Dunia, ilitubidi kupingwa na kuteswa na mataifa matatu. Lakini, hata katika mashindano hayo, ilitubidi kuweka sawa masharti ya malipizi katika upeo wa Dunia. Hii ndiyo jinsi tulifanya upeo wa ushindi katika njia ya kwanza ya miaka saba, ambayo iliisha mwaka 1967. Sasa tuko katika njia ya pili ya miaka saba, ambayo ilianza mwaka 1968.

Sababu ambayo inatupasa kuwa washindi katika njia ya malipizi ni kwamba inatupasa kukomboa upeo wote uliopotezwa kwa kuanguka kwa Adam na Hawa pia wakati wa Yesu. Tunapaswa kukomboa kila kitu, vyote ki-ndani hata ki-nje. Kanuni ya Mungu mnayojifunza

inakukumbusha yale yote yaliyotimilizwa katika historia, lakini hata kitabu hiki hakiwezi kufafanua namna ya kuikomboa kabisa. Sasa ninajitahidi ili kufaulu kuvumbua njia hiyo.

Hivi sasa huko Korea, hakuna nguvu yoyote itakayoweza kulishinda Kanisa la Umoja; Kanisa letu haliwezi kufutiwa mbali na Dunia hii. Tumeshatimiliza kabisa upeo wa ushindi; msingi wa ushindi. Hata kama upande wa uovu utapiga Kanisa la Umoja, Mungu anaweza kulilinda, na Shetani hawezi kulisuta. Hii ni mtiririko muhimu (yenye thamani) wa ushindi ambao ulitimilizwa katika kipindi cha miaka 21 iliyopita chini ya uongozi wangu. Ni furaha kubwa kwa historia nzima, Dunia pia ulimwengu ya kwamba wakati wa siku za mwisho, Kristo aliye hai, ambaye Mungu alimtafuta kwa miaka yote 4000 ya Agano la Kale pia miaka yote 2000 tangu kupaa kwa Yesu, amehitimisha upeo uliopotea. Hakuna Injili nyingine ingeweza kuwa ya kustaajabisha zaidi ya hii. Hakuna kitu kingine kingewezesha raha ya kuzidi nafasi ya kukamilisha masharti yote ya malipizi ya aina ya wima pia mlalo hapa Duniani.

Ukombozi kwa kupitia malipizi inapasa kutimilizwa kwa njia inayokwenda kinyume. Ndani ya familia ya Adam, Adam aliyeanguka anapaswa kukombolewa kwa kupitia umoja kati ya Kaini na Abeli. Kwa sababu hiyo, ila tunawakomboa Kaini na Abeli, hatuwezi kuwakaribisha Wazazi wa Kweli kama Masihi. Kwa hivyo, Bwana wa Ujio wa Pili, ambaye ameungana moja kwa moja na Roho ya Mungu, alipaswa kupitia njia ya mashaka na kusulubiwa kwa Yesu. Kwa taabu sana ilimbidi kutatua matatizo yote pia kuwa sadaka hai ili kupata ushindi. Kama sivyo, msingi wa ukombozi hauwezi kutekelezwa. Hivyo, njia ya kwanza ya Masihi ilikuwa njia ya kusakamwa toka pande zote.

Shutuma za aina hiyo hazijawahi kuonekana huku Japan. Lakini kule Korea, hali ilikuwa ngumu ili mpango wa Mungu uweze kukamilishwa

katika kiwango cha Dunia chini ya uongozi wa utume wangu. Kwa sababu hiyo, Kanisa la Umoja lilianza njia yake gerezani.

Kanisa la Kikristo la mwanzo lilianzishwa wapi? Nalo pia lilianzishwa gerezani. Historia ya Kanisa la Kikristo, au Israeli ya pili, ilianza katika nafasi chungu ya udhalimu pia kufungwa. Ili kuikomboa, tunapaswa kuilipia malipizi. Kwa hivyo, Kanisa la Umoja lilianzishwa gerezani, ili Mungu apate kufanya kazi yake moja kwa moja na Kanisa letu. Tofauti ni kwamba, pale Yesu alipofungwa, wanafunzi wake walitoroka pia kutawanyika. Lakini nyinyi sasa mnahitaji kwenda kinyume. Hata katika hali ya kutisha, kukatisha tamaa, wote tungeungana kwa pamoja pia kusimama kwa ujasiri mbele za kifo. Ilichukua sawa na miaka 21 kuibuka toka upande wa chini kabisa, kupitia maongozi ya Mungu ya wokovu. Kwa asili, kama dini kiongozi katika taifa teule lililomkubali Masihi, ukombozi ungechukua miaka saba tu. Kwa kuwa hatuwezi kukubalika, ilitubidi kupitia njia ya miaka 21. Mnafahamu kiasi juu ya njia ya kwanza ya miaka saba baada ya mwaka 1960, lakini sio msingi kamili. Nyuma ya njia hii kulikuwa na historia ya familia ya Mungu pia historia ya kabila lililokuwa chini ya Mungu. Ili mwelewe historia hii, mngehitaji kupokea Baraka. Siwezi kufunua msingi huu msipopokea na kurithi upeo wa ushindi wa Baraka. Mnapofahamu njia hii kikamilifu, mtajihisi ni kwa jinsi gani historia ya ukombozi ilivyokuwa chungu. Kwa hivyo, tunapaswa kung'amua ni kwa kiwango gani Baraka ina thamani.

**Rithini utamaduni wa Yesu:**

Kama tunataka Baraka, kwanza tungejitokeza juu ya namna halisi ya kuishi kwa ajili ya matakwa ya Mungu tu. Hapo Yesu alisali kule Gethsemania, aliomba ili mapenzi ya Mungu yafanywe sio yake mwenyewe. Yeye hakuchagua njia ya msalaba kwa sababu ya kujipendekeza (ya nia yake pekee). Msipokuwa, kama Yesu, na imani ya kuwa na uwezo wa kushinda matatizo yote ya uhai na kifo, hamwezi kupokea wala kutembea njia ya ukombozi. Je, mnayo imani

kiasi cha kutosha cha kuweka wakfu (kutabaruku) maisha yenu kwa ajili ya matakwa (mapenzi) ya Mungu? Kama mnafuata njia hii, mngehitaji kujua ya kwamba hamwezi kuitembea peke yenu; mnapaswa kuweza kuhusiana na watu wote, na kutuliza wale ambao watakuwa wanawafuata katika njia hii.

Je, mko tayari kweli kutoa mhanga maisha yenu? Hamwezi kufikiri, “Mimi ndiye msichana mwenye sura nzuri, ninaweza kupokewa kwa raha popote niendapo; na sina kasoro maalum. Msichana kama mimi siwezi kufanya kazi yoyote ya kujitoa mhanga.” Au, “Mimi mwanaume mwenye mwili mkubwa, pia sura nzuri, mwenye kutoka kwenye familia maarufu. Chochote kile ninachokitaka naweza kukipata kwa urahisi sana. Kwa hivyo, kuwa mwanaume mzuri kama hivyo, siwezi kufanya kazi ya kujitoa mhanga, ngumu namna hiyo.” Zaidi ya hapo, msiwe na uhasama juu ya kutembea njia ya kujitoa mhanga.

Wakati Yesu alikuwa anajitwika msalaba, yeye angeweza kujutia hali yake na kusema, “Isingenibidi kufanya jambo kama hili. Sijaoa, ingawa mimi ni mwanaume mwenye umri wa miaka 33. Utume pia thamani yangu bado haijatimilizwa.” Lakini Yesu hakuweza kuwaza hivyo. Kifo chenyewe hakikuwa tatizo kwake; alikuwa tayari kutoa mhanga maisha yake, na uzito wa msalaba ambao alijitwika haukuweza kumuogofya. Ingawa kimwili alianguka chini, yeye hakuyumbayumba moyoni mwake, kwa sababu ya ushupavu wake mkubwa. Hakuna mtu mwingine katika historia ambaye alikuwa na ushupavu wa nguvu uliounganishwa na Mungu kama huo, na kwa sababu ya uwezo huo mkubwa wa Yesu, historia wa wanadamu ilichukua mwelekeo mpya. Hii ikawa mahali halisi pa Mungu kuanzia upya Duniani.

Kumepita miaka elfu mbili toka wakati ule, lakini roho ya yesu haijafa. Badala yake, ilirithiwa na mamilioni ya watu. Raha gani tunaweza kuwa nayo leo – kwa kurithi utume (mkubwa) muhimu kama huo – utamaduni wa Yesu! Kwa hivyo, haidhuru hata kama tunapoteza maisha yetu. Tungehitaji kulia kwa machozi toka giza la

kifo na kuangamiza giza hilo kwa anga ya roho ya Mungu. Tungeifanya anga hiyo kumulika Duniani pote. Tunapaswa kuwa mwanaume na mwanamke wa aina hiyo. Hili ndilo shindano.

Kwa asili, anguko la mwanadamu lilimaanisha kifo; wokovu unamaanisha kushinda kifo. Kama tumeamua kuokoka, tungekubali kujipendelea kuwa jasiri. Tukishinda Dunia itaelekea upande mpya. Tungehitaji kusisimka! Je, mnao uhakika wa kushinda matatizo ya uhai na kifo? Nilishakutana na mashindano ya uahi na kifo mara nyingi sana – mamia, maelfu, hata makumi ya maelfu. Ingawa ninaweza kukutana na taabu pia mashaka, ingawa miguu yangu inaweza kukatwa na macho yangu kung'olewa, hata nikikatwa kichwa, bado nina uamuzi mkali wa kutimiza utaratibu nilioanza. Sadikisho langu ni kamili.

**Ushindi ambao Mungu anataka:**

Siku nyingine, kundi la watu wanaokaribia 50 toka Japan wakaja Korea na kuzuru Kiwanja Takatifu cha Pusan. Ni karibu na makaburi, katika eneo la mawe mengi ambamo hakuna mtu anaishi. Mahali hapo nilijenga kakibanda kadogo kwa makaratasi na matope tangu miaka mingi. Ilikuwa mbali na mahali adhimu, lakini hata wakati nilipokuwa nikilala humo, nilitembea njia ya mtoto mwenye utawa mbele za Mungu kama mtoto wake. Upekuzi wangu ulikuwa upeo mnene wa ndani ambao hata mtu mwingine mmoja aliwahi kufikia. Wakati ule, sikuwa na miliki yoyote ya nje, sikuwa na fedha. Nilikuwa na ndevu pia uso usiooshwa, wa nguo za asili za Mashariki na Magharibi. Lakini pale popote nilipokwenda, nilizungumza juu ya mambo makubwa, vitu ambavyo vilikuwa vikubwa kuliko mzinga, yenye mshindo mkubwa kuzidi kombora lenye vichembe vikubwa mno kiasi cha kwamba kila mtu aliesikia alishtuka na kukimbia mbali.

Nilivumilia mkasa wa kutisha maisha yangu yote, lakini hamwezi hata kunielewa. Ingechukua kama miaka 50 kuueleza. Lakini, neno langu la mwisho ni kwamba haidhuru taabu unaweza kupata katika shughuli zenu, na haidhuru kiasi gani mtadhulumiwa na mazingira yenu,

ingewabidi kuwa na uwezo wa kusimama daima mbele ya uso wa Mungu.

Ingawa Yesu aliacha Dunia kwa ajili ya msalaba, upeo wa mtoto mwenye utawa alichapa ndani ya roho ya Mungu ulibaki, na Mungu alilazimishwa kuijibu. Ingawa Yesu hakutafuta mjibu wowote toka kwa Mungu, lakini roho ya Mungu haikuweza kujizuia kumfikia. Yesu alikuwa mtoto wa kweli wa kwanza wa Mungu baada ya miaka 4000 ya historia ya kibiblia.

Kuna karibu watu 300 waliokusanyika hapa. Kama wote mna uamuzi wa kufanya kama Yesu, majimbo 43 ya Japan yatakombolewa. Ushindi unaotokana na uamuzi wa ndani (kiroho) unaofanywa mwanzoni mwa mradi, sio popote katikati. Mngepaswa kuelewa hili.

Hata mkiwa na uwezo wa kupata ushindi juu ya mamia ya hali ya uhai ya kifo, mnahitaji ushupavu mkubwa zaidi kabla ya kuweza kushinda ushindi wa milele ambao Mungu aliutaka, sehemu ambayo iko mbali na Shetani.

Mnaweza kujiuliza kama mateso yenu katikati ya mazingira ya uhasama yatasaidia utaratibu wa ukombozi. Lakini tayari nilishafikiria/hesabu hizo kwa uhakika, ili kile ambacho Kanisa la Umoja inafundisha iweze kusisimua historia na kupata kuwa historia ya kweli. Ninafundisha kile ambacho hata mtu mmoja hakuweza kudhania.

Huko Japan kila mtu anaongea juu ya Kanisa la Umoja. Wanajiuliza kwa sababu gani vijana hawa wanaonekana kama wanapoteza ujana wao, wanatembea njia ya mateso. Baadhi yenu hata waliingia Chuo Kikuu cha Tokyo pia walisifiwa na ndugu zenu; walakini, kwa sababu mlijiunga na Kanisa la Umoja, familia zenu ziliteketezwa (zilitekwa). Kuna wengi kati yenu ambao wako katika hali hiyo. Lakini kama mnatarajia kuwa wanaume na wanawake maarufu, mngefanya kazi na ulingo wa Dunia nzima. Haidhuru kiwango gani mnaweza

kuteswa Japan, mateso haya hayatoshi kukuwezesha kuingia katika mtiririko kamilifu wa Mungu.

Nini Kanisa la Umoja? Ni Kanisa ambalo upekuzi wake ni kufanyiza upeo ambao unaweza kutuingiza katika mtiririko kamilifu wa Mungu. Kwa hivyo, kwa kuwa sasa mnafahamu hivyo, mnapaswa kuzingatia thamani hiyo kubwa maishani mwenu.

**Njia ya udhalimu:**
Wakati wa Yesu, watume wakuu watatu, watume 12, wanafunzi 70 na 120 wote wakawa wadanganyifu. Kwa sababu hiyo, mwishoni ilimbidi Yesu apitie njia ya msalaba. Inatupasa kulipia tendo hili pia kuazimu kurudi kwa Mungu kwa kuhatarisha maisha yetu. La sivyo, njia ya ukombozi haitawezekana. Tunapaswa kupitia njia ya udhalimu na kuchukua majukumu ya kwango cha Taifa. Tunapaswa kuwa dhahiri kukomboa vitu vyote kikamilifu katika vizazi vitatu. Vizazi vitatu vinahitajika kwa kuwa tatu ni namba katika Kanuni, pia msingi wa nafasi nne unafanikishwa katika hatua tatu. Kwa kusudi kama hili, tunapaswa kustahimili dhuluma pia kushinda vizuizi vyote.

Yesu alikuja kama Mzazi wa Kweli au Baba wa Kweli, lakini Yuda alimsaliti. Katika tendo lake la uhaini, walimwengu wote waliwakilishwa. Kwa njia yake, wanadamu wote, kuwa kama uzao wa msaliti, walimsaliti Mzazi wao wa Kweli. Kwa sababu hiyo, inatupasa kufanya mchango wa malipo kwa kukomboa tendo la kumuuza Mzazi wa Kweli.

Kwa sababu ya sarafu 30 za fedha, mtu mmoja alimfukuzia mbali na Dunia hii Mzazi wa Kweli na kuzuia kabisa maongozi ya Mungu ya miaka 4000. Wakati uleule, Shetani alishurutisha (alishinda juu ya) Dunia. Kwa kulipia tendo hili, tunapaswa kutoa idadi hii ya fedha na namba tatu – katika miaka minne, kama gharama ya kumuuza Mzazi wa Kweli. Miaka minne zinawakilisha Mashariki, Magharibi, Kusini na Kaskazini. Katika Korea, hii inamaanisha kwamba tunapaswa kulipa won 3000 (sawa na $30) kila mwaka kwa miaka minne. Pesa hizi

zinapaswa kupatikana kwa jasho na machozi yako/yenu, na unapopata hizo fedha inakubidi/inawabidi kufikiri juu ya nia ya Mungu zaidi ya maisha yako/yenu binafsi. Fedha hizo zinahitaji kutolewa kwa Mungu kwa moyo kama huo.

Zaidi ya hapo, wafuasi wakuu watatu wa Yesu walihitajika kuungana naye kwa moyo, lakini badala walimtoroka. Watume 12, na 70 na wafuasi 120 wote pia (wakawa wadanganyifu) hawakuwa na imani. Kwa sababu hii, katika njia ya malipizi, tunapaswa kuyakomboa haya yote. Vivi hivi, kila mmoja wetu yatupasa kupata watoto wa kiroho watatu, na msingi wao, kupata wafuasi 12, halafu 70 na halafu tena 120. Hii ni kile ambacho nilikuwa nakifanya kwa miaka 21 iliyopita. Kwa kuwa Yesu hakuweza kukamilisha kusudi/lengo hili Duniani, Yeye na Mungu walishindwa na huzuni.

Utume wa Kanisa la Umoja ni kuondoa huzuni hizo. Hii ndiyo njia/kipito yetu/chetu kikanuni. Yatupasa kukomboa kabila zetu, kwa kuimarisha nafasi yetu kama mababu wapya. Na yatupasa kukomboa Japan, Asia na hata Dunia nzima, hivyo kuendeleza maongozi ya Mungu ya ukombozi na kiwango cha Dunia nzima.

**Ndoa Takatifu:**

Kwa ajili ya Ndoa Takatifu ya mwaka 1960, ilitubidi kukamilisha masharti ya malipizi ya miaka 4000 kibiblia kabla Yesu na historia ya miaka 2000 baada ya Yesu. Maana ya Ndoa Takatifu hiyo ilikuwa ya Dunia nzima pia kiulimwengu, lakini ni watu wachache tu ndio waliishuhudia. Kwa wakati ule, bado tulikabiliwa na udhalimu mkali mno.

Kipindi cha maandalizi toka 1953 hadi 1960 kilikuwa wakati wa udhalimu mkali mno. Wakati huo, zaidi ya watu milioni 3, madhehebu ya kikristo makuu matatu, na awamu za Serikali tatu katika Korea walitupinga. Ijapokuwa hivyo, ilitubidi kuleta ushindi kwa kukamilisha masharti ya malipizi. Ile ilikuwa mahali pa nyuma (msingi) kwa Ndoa Takatifu yangu ya mwaka 1960.

Siku ile ya harusi ilidhihirisha maisha ya Kanisa la Umoja. Ilikuwa tukio kubwa kwa Dunia na ulimwengu. Masharti ya malipizi wima yote na kiwango cha Dunia nzima yalikombolewa kimlalo Duniani kwa kupitia utume wangu, kwa sababu nilileta ushindi kiroho na kimwili kwa mara moja. Sharti mmoja ilikuwa kukomboa wafuasi watatu kabla ya Baraka yangu – kwa kuwakilisha wafuasi watatu waliomtoroka Yesu miaka 2000 iliyopita.

Adam na Hawa walianguka kama mume na mke wachumba. Kwahiyo, ukombozi hauwezi kufanyika kwa mtu mmoja peke yake, wokovu hauwezi kukamilika kwa mume peke yake, wala mke hawezi kwenda Mbinguni peke yake. Kwa hiyo, inawapasa mume mmoja na mke mmoja kutatua tatizo. Kwa kufanya kipeo cha Adam na Hawa kama Wazazi wa Kweli Duniani, yalitupasa kukamilisha sharti na msingi wa kuchumbia wa wafuasi watatu.

Nia ya Mungu ilikuwa kukomboa familia ya Adam, lakini ulegevu wa Kaini na Abeli ulihamisha maongozi kwa familia ya Nuhu. Kwa njia ya familia ya Nuhu, binadamu wote Duniani walihukumiwa kwa gharika, ili kung'oa kabisa mwingilio wa Shetani wakati wa anguko. Hii ilikuwa maongozi ya Mungu kwa wokovu Duniani. Baadaye, jukumu lilihamishwa kwa familia ya Abrahamu, Isaka na Yakobo, na hata baadaye kwa Musa na tena Yesu. Hivyo twaweza kuona ya kwamba, maongozi ya wokovu ya Mungu yaliongezewa urefu mara nyingi. Kwa sababu hiyo, yatupasa kulipia njia hiyo. Ili kulipiza katika kiwango cha familia ya Adam na wawe kama Wazazi wa Kweli, kwanza yatupasa kukomboa watoto watatu wa Adam.

Kwa uhakika Yesu alihitaji wafuasi watatu kuwakilisha malaika wakuu watatu katika Bustani ya Eden. Kwa kuwa malaika wakuu hawa hawakuungana kabisa na Adam na Hawa na kuwatumikia, Dunia potovu ikaja kuwepo. Ili Wazazi wa Kweli wakamilifu kukamilisha nafasi yao, wanahitaji wafuasi watatu, sawasawa na malaika wakuu, ambao wanaweza kuwatumikia kabisa. Bila hili kufanywa, Shetani hawezi kung'olewa katika Dunia hii.

Historia nzima ya watu wa aina ya Kaini kutotii watu wa aina ya Abeli inakombolewa kwa njia ya wafuasi watatu wa Bwana. Wanawakilisha malaika wakuu watatu katika ulimwengu wa kiroho na Kaini katika vipindi vikuu vitatu vya maongozi – ni kwamba vipindi vya Agano la Kale, Agano Jipya na Agano Kamilifu – au Kaini kati ya familia ya Adam, Kaini wakati wa Yesu pia Kaini wakati wa Ujio wa Pili. Kwa kulipiza kabisa historia kama hii, Bwana wa Ujio wa Pili anaemwakilisha Yesu, ambae mwenyewe amemwakilisha Adam wa kwanza, yampasa kukuza wafuasi watatu wakuu ambao wanamwakilisha Kaini watatu.

Katika ulimwengu wa kiroho, kuna malaika wakuu watatu. Katika Dunia ya kimwili, watoto wa kiroho watatu wanahitaji kufuata Abeli wao kikamilifu; wafuasi watatu wanahitaji kubaki waaminifu ingawa kutakuwepo na udhalimu. Kiwango hiki kiliimanishwa April 1960.

Kwa kuwa njia ya ukombozi ni njia ya ugeuzi, wale ambao wako katika nafasi ya watoto yawapasa kubarikiwa kwanza. Wafuasi watatu au watoto watatu yawapasa kukamilisha sharti hili.

**Kubarikiwa kwa wafuasi 12:**
Baada ya kuchumbisha wafuasi watatu ambao walimaanisha ufufuo wa watoto wa kiume watatu wa Adam – Kaini, Abeli na Seti – Wazazi wa Kweli walisimama kwenye nafasi ya Wazazi wa uhakika, jinsi ilivyotangazwa kwenye sherehe ya Ndoa Takatifu ya 1960. Mungu aliichukia familia ya Adam, lakini Wazazi wa Kweli walikuwa na uwezo wa kuendeleza umoja baina ya wazazi na watoto kwa mara ya kwanza Duniani. Hii ilifanywa mwaka 1960 kule Korea. Kwa hiyo, lilikuwa tukio la pekee kihistoria ambalo lilianzisha historia mpya.

Aprili 1960, hatua ya kwanza ya Baraka na msingi wa namba 12 ulikamilika. Kihistoria, hii ni sawa na kukomboa wafuasi 12 wa Yesu. Biblia inaongea kuhusu milango 12 ya Mbingu; namba 12 ni kuu katika historia ya Israel. Basi kwa kulipizia historia hii tu ndiyo kipeo

cha Ukristo, ambao uliendeleza utume wa kiroho tu, inaweza kuotesha mzizi hapa Duniani kwa vyote kiroho na kimwili.

Sikitiko kubwa la mungu lilikuwa kwamba toka anguko yeye hakuweza kuhifadhi hata sehemu moja ya kuweka mguu kati ya Dunia hii kwa kiwango cha mtu mmoja, kiwango cha familia, au na kiwango cha taifa. Ili kuponya sikitiko hilo, yatupasa kwanza kukamilisha ukombozi wa viwango vya mtu mmoja pia familia.

Kulikuwa na familia 12 toka Adam hadi wakati wa Nuhu, wakiwemo Kaini, Abeli, Shemu na Shamu. Tena kuna familia 12 toka Nuhu hadi wakati wa Abrahamu, wakiwepo Isaka na Yakobo. Ufufuo wa watu 12 katika Baraka unamaanisha ufufuo wa mababu wote kuanzia wakati wa Adam hadi Abrahamu. Kwa maneno mengine, sharti ya malipizi wima ilikamilisha kimlalo. Kwa hivyo, ingawa kulikuwa na vizazi 10 toka Adam Nuhu, kwa maongozi kulikuwa vizazi 12 endapo Kaini na Abeli wanahesabiwa. Kwa hiyo, katika mtiririko thabiti, wafuasi 12 walibarikiwa kuwa kama sharti ya malipizi.

Hii ilileta ushindi kwa nafasi ya pili, ambao kila wakati Shetani alikuwa anasuta. Familia ya Nuhu iliwakilisha ile ya Adam. Kwa kuwa niliweka msingi wa kufufua familia ya Nuhu, nilikuwa na uwezo wa kufufua vizazi 12 toka Adam hadi Nuhu, wakiwemo Kaini na Abeli. Ufufuo wa hao katika Dunia ya kiroho na ukombozi wa Dunia ya kiroho vilikamilishwa kwa msingi wangu Duniani.

**Aina Tatu za Familia:**
Mwinuo kwa kukomboa familia ya Adam, familia ya Nuhu na familia ya Yakobo uliweza kufanyizwa tu kwa baraka ya familia ya Yakobo. Kwa mara ya kwanza katika historia ya wanadamu, katika Baraka ya viungo 36, uhusiano huu wima ulifanywa kabisa kimlalo. Kundi la kwanza na la pili na la tatu la familia zilizobarikiwa zinadhaniwa moja kwa moja kama familia ya Adam, familia ya Nuhu na familia ya Yakobo. Familia ya Adam iliwakilishwa na kundi la kwanza la wabarikiwa viungo 12, wale ambao tayari walikuwa

wameshaoana kwa kuongozwa na tamaa zao binafsi. Familia ya Nuhu iliwakilishwa na kundi la pili la wabarikiwa viungo 12, wale ambao hawajaoa au kuolewa, lakini walikuwa wanatafuta ndoa na upendo. Familia ya Yakobo iliwakilishwa na kundi la tatu la wabarikiwa viungo 12, wale ambao walikuwa bikira/watakaso. Kwa njia ya Baraka hii ya viungo 36, hazina ya Kanisa la Umoja pia msingi wa Umoja wa Mbingu na Dunia ulidhihirishwa. Hii ilileta ushindi mlalo kwa historia wima, ambayo ilikuwa imejazwa na malegevu mengi yaliyomsababishia Mungu maumivu makali. Tena ushindi huu uliunganisha Dunia ya kiroho na Dunia ya kimwili. Sasa Mungu ana mahali pa kutegemezea mguu hapa Duniani.

Sasa ambapo Mungu anaweza kufanya makao Duniani, ustawi na kiwango cha Dunia nzima hapa Duniani uliweza kuanza. Katika miaka saba baada ya 1960, Ujio wa Mungu Duniani ulitaka kukamilika. Hii ilihitaji ukombozi wa watoto.

Kwa zamani, ma-Kaini hawakuweza kuwatii ma-Abeli, na kwa hivyo kuviongezea urefu kwa maelfu miaka historia ya binadamu. Ili kukomboa hii, Kaini na Abeli wangehitaji kuungana kati ya familia moja kwa wakati huu. Hii ililipiziwa kwa Baraka ya viungo 72, 36 wakiwakilisha familia ya Kaini na 36 wakiwakilisha familia ya Abeli. Kwa njia ya Baraka hii, msingi wa nafasi nne ambao mababu zetu hawakuweka, ulitimilizwa, na Shetani alilazimishwa kurudi nyuma.

Kufuata Baraka ya viungo 72, Baraka ya viungo 124 iliweka msingi wa ustawi Duniani kote na kiini cha Wazazi wa Kweli. Viungo 124 ni kuwakilisha vichwa vya mataifa yote ya Dunia. Kwa ajili ya Yesu kuanza ukombozi wa kiroho na kiwango cha Dunia nzima, alihitaji wafuasi 120. Vilevile, kama kichwa cha Kanisa la Umoja, yalinipasa kuanzisha njia yangu thabiti na wabarikiwa viungo 124. Hii nilikamilisha kadiri ya miaka 21. Baada ya kupata watu ambaye alikuwa anawatafuta, Mungu alianza ukombozi wa vitu vyote. Kuwekwa kwa viwanja vitakatifu inamaanisha baraka ya vitu

vyote. Hivyo, viwanja vitakatifu viliwekwa katika nchi 40 Duniani kote mwaka 1965. Hii ilikuwa kikomo cha ustawi/manzili wetu/yetu.

**Azimio la Siku ya Mungu:**
Moja ya siku za kustaajabisha zaidi ni Siku ya Wazazi. Sisi watu duni hatukuwa na uwezo wa kuwa na wazazi ambao wangeweza kumfuarhisha Mungu. Lakini toka Wazazi wetu wa Kweli wakombolewe, raha imewarejea Mungu na mtu.

Halafu tuliweka Siku ya Watoto. Mpaka sasa, watu hawakuweza kusheherekea siku hizo za kustaajabisha kwa sababu hatukuweza kukamilisha njia ya ukombozi. Lakini sasa Injili kubwa imeshakamilishwa kihistoria.

Kwa kumaliza, Siku ya Mungu ilitangazwa Januari 1, 1968. Azimio la Siku ya Mungu liliwezesha kuwepo kwa Mungu Duniani kuwezekana na iliyakinisha endeleo la kila siku ya Kanisa la Umoja. Sasa tunaweza kujitahidi kwa ukombozi wa Dunia kiroho pamoja na Dunia kimwili, na hata ukombozi wa Jehanamu juu ya msingi wa ukweli wa Kanuni. Kwa kuwa Siku ya Mungu ilitangazwa, tunaweza kurudi katika hali ambapo Jehanamu na Shetani hawana shikilio. Siku ya Mungu ilipotangazwa, utume wangu ulikamilika.

Kwa miaka mingi nilidhulumiwa na Korea pia na makanisa madhubuti kama vile Yesu alivyodhulumiwa na viongozi wa Uyahudi. Kwa njia ya Injili yake mpya, ilimpasa Yesu kuvumbua njia ya Kanuni kwa kushinda ukubali wa Uyahudi na kuondoa udhaifu wao. Jaribio la kuimarisha Uyahudi wa pili, alitwaa Ukasisi wake wa miaka mitatu kwa umma. Hii ni pamoja na kuinua maongozi toka kiwango cha mtu peke yake hadi kiwango cha familia, na toka pale hadi kiwango cha kabila pia taifa. Yesu alitaka kufanyiza msingi wa ushindi daima kwa vyote kiroho na kimwili ili Israel iweze kukombolewa kutoka kwa Shetani. walakini, alizuiliwa kufanya hivyo.

Vile vile Yesu alivyodhulumiwa na viongozi wa Uyahudi, nilidhulumiwa na makanisa madhubuti hapa, na baina yake, ilinibidi kupigana kwa kukomboa kila kitu. Mwaka 1945, hali ilinibidi niende Pyong Yang, mji mkuu wa Korea Kaskazini, kati ya kambi la Shetani. ilinibidi kuondoka Seoul na kuacha nyumbani, ambapo Mungu alikuwa anabariki na pale ambapo alikuwa na msingi halisi na kwenda katika makao makuu ya adui wa Mungu. Bila kushinda sharti ya masuto ya Shetani katika hali hii, nisingeweza kuanza kwa mara ya pili. Hii ndiyo sababu nililazimishwa kuishi gerezani katika nchi ya kikomunisti.

Kule gerezani, ilinipasa kupata wafuasi 12 kwa kukomboa hali ya Yesu, ambaye alitorokwa kabisa na wafuasi wake wote wakati alikuwa gerezani. Kwa njia hii, historia mpya iliweza kuanza toka gerezani. Baada ya kukamilisha sharti hili, niliweza kurudi Kusini, kule ambapo bado ilinibidi kustahimili aina yote ya masuto na uzuio toka makanisa madhubuti. Tulifanya kazi kwa miaka mingi kwa kuimarisha kundi jipya ambalo lingeweza kuyadizi makanisa madhubuti yote, ili kutimiza maongozi ya Mungu. Hili ndilo Kanisa la Umoja huko Korea.

Miezi michache iliyopita, tarehe 10 Sept. 1968, tulifungua Academy House na tuliwaalika viongozi wote wa ki-Kristo. Wale walioitika ni viongozi wa makanisa ya ki-Kristo walioipinga kwa nguvu Kanisa la Umoja. Kadiri ya watu 40 walikuja. Wao wote walionekana wenye kiburi sana, lakini niliwapokea kwa ujasiri. Kwa kweli, nilifurahi sana kwa kuona muda kama huo umefika. Viongozi hawa wa ki-Kristo walikuwa wanalipinga Kanisa la Umoja kwa miaka mingi; walizoea kufikiri kwamba sisi tulikuwa watu hafifu, maskini na duni. Lakini sasa waliweza kuona ya kwamba Reverend Moon hakuwa mtu wa jinsi walivyomfikiria. Mara hii, waliweza kunipokea pia kutambua Kanisa la Umoja.

Kanisa la Umoja limekuwa dai zito kwa Korea. Sisi ni kundi moja linalohofiwa zaidi na ninatazamiwa kama kiongozi mmoja wa kuogofya. Makanisa madhubuti hayakuweza kubishana na Kanisa la

Umoja.  Hayakuweza kushinda elimu ya kanisa letu.  Kwa hivyo, sasa wanashauriana kutojishughulisha na Kanisa la Umoja.

**Msingi wa Ushindi:**
Kwa kustahimili udhalimu, tulivumbua njia ya ukombozi.  Ingawa Dunia nzima inatupinga, tutakuwa shujaa.  Haidhuru mara ngapi tunaweza kufa kwa ajili ya Mungu, kwa uhakika tutafanya mapenzi ya Mungu.  Hii ilikuwa kitendawili kwa makanisa madhubuti.  Nimefumbua matatizo yote ya kihistoria isiofumbulikana ambayo yalimkabili Mungu katika historia ya miaka 6000 kibiblia.

Ustawi umefanyizwa.  Hata kama nikifa sasa, elimu ya Umoja itadumu Duniani.  Haidhuru kiasi gani nchi nzima ya Japan imejihamasisha kushindana nasi, elimu ya Umoja haitashindwa kamwe.
Je, Mungu anaihitaji Japan?  Yeye haihitaji kwa sababu yake mwenyewe.  Anaihitaji kwa sababu anaihitaji Dunia -  Dunia ya kiroho, Dunia ya kimwili na ulimwengu.  Mungu alitangulia kuumba mazingira ya Dunia, akiwa anaandaa kila kitu kwa mara ya kwanza.  Kwa hivyo, kama tutafanya sehemu yetu ndogo sasa, Dunia nzima itaongozwa.  Tunaishi katika wakati kama huo.

Nyie vijana msingeweza kamwe kuwaza kwamba Mungu hayupo.  Kwa uhakika Mungu yupo, lakini yeye siyo Mungu wa kuwazika tu bali ni Mungu anayeshughulika katika maisha yetu.  Yeye sio mwenye kuhisia tu, ni mwenye matendo.  Ajabu gani hii!

**Kiwango cha Baraka:**
Bila kukamilisha njia ya ukombozi na kiwango cha mtu peke yake, familia, kabila, taifa na ulimwengu, vivyo hivyo kuimarisha upeo ambao Shetani hawezi kuusuta, hatutakuwa na uwezo wa kuweka sharti kwa ajili ya Baraka.

Katika 1960, tulifika kiwango cha juu cha hatua ya ukuaji, ambapo Adam na Hawa waliangukia.  Ili Wazazi wa Kweli wafikie mtiririko wa ukamilifu, kipindi cha miaka saba kilihitajika, kwa kuwakilisha hatua saba.  Ile ilifanyiza njia ya kwanza ya miaka saba.  Tunapoingia upeo

wa ukamilifu tunaenda kwenye mtiririko wa utawala wa moja kwa moja wa Mungu. Utawala wa moja kwa moja una maana kwamba kuwa katika uhusiano wa moja kwa moja na Mungu kwa ndani na kwa nje; huu ndiyo upeo wa utawala wa rohoni pia maishani.

Katika 1960, Baraka ilifkiwa, lakini sio kiwango cha kweli cha ukamilifu; bado Dunia ilikuwa katika mtiririko wa utawala wa Shetani. Kwa hiyo, Shetani alikuwa na uwezo wa kushambulia Familia ya Kweli Takatifu. Hata hivyo, tumeshinda uzuio wote katika miaka hiyo saba, kwa kufanyiza Siku ya Wazazi, Siku ya Watoto, Siku ya Vitu Vyote na mwisho wake Siku ya Mungu. Kwa hiyo, upeo wa ukamilifu uliimarishwa kabisa Duniani.

Mungu alikuwa anatafuta siku ambapo bwana arusi mmoja na bibi arusi mmoja wangekutana, kwa kushinda uzuio wa Shetani. kwa miaka 2000 iliyopita ya historia ya Ukristo, bwana arusi alikuwa Yesu ambaye alikuwa anafanyia kazi Mbinguni, na Roho Mtakatifu, ambaye alikuwa anawakilisha tabia ya kike ya Mungu, alikuwa anafanyia kazi Duniani.

Lakini, kwa kupitia Kanisa la Umoja, Mbingu na Nchi wameunganishwa kabisa, kwa kuondoa kuwepo kwa Shetani kama kizuizi kati ya Mbingu na Nchi. Kusudi kuu la watu wa Dini limeshakamilishwa. Kama kabila hii itakua siku kwa siku, itakuwa taifa na baadaye itapanuka hadi kiwango cha Dunia. Toka hapo, taifa mpya, Israel wa tatu, itaanzishwa.

Ingawa nyie ni wa-Japan, hamko tena watoto wa mababu wa ki-Japan, ila watoto wa Mungu katika ukoo wa damu mpya. Kanisa la Umoja limefanikisha. Tunasimama katika nafasi tofauti. Hii ni mtiririko wa ushindi ambao unaondoa masuto ya Shetani.

Mnasimama katika nafasi gani? Msipofikia kiwango cha ukamilisho cha hatua ya kukua, hamtastahili kuwa wabarikiwa. Wakati wa anguko, mme mmoja na mke mmoja walifukuzwa nje ya Bustani ya Eden. Kwa sababu hiyo, katika njia ya ukombozi, mme mmoja na mke

mmoja wanapaswa kushinda mazingira ya uhasama. Hii ndiyo maana ya Baraka.

Siku zangu za Mungu, Wazazi, Watoto na Vitu Vyote zilitangazwa na kiwango cha Dunia nzima pia na kiwango cha ulimwengu. Mnaweza kubarikiwa na kushiriki katika mtiririko kama huo, walakini hamjapitia njia ile ile niliyofanya. Kwa kweli, kama mababu wa kweli wa ukoo mpya, lazima mfanyize Siku yenu pekee ya Wazazi. Tena, mngehitaji kufanya Siku yenu pekee ya Watoto, Vitu Vyote na Siku ya Mungu. Vitu hivyo vyote waumini wa Kanisa la Umoja wanatakiwa kuvifanya. Hii ndiyo sababu ilitupasa kuanza njia ya pili ya miaka saba.

Ingawa nyie ni ukoo wa anguko, mngehitaji kuzidi kipeo Adam na Hawa, kwa kusonga mbele kwa ushujaa/ujasiri kwa kushinda masuto ya Shetani. Hii ndiyo kile kinamaanishwa na endeleo la kimwili. Sio sisi wenyewe tu, lakini ni Dunia nzima ndiyo ingebidi kufanya hivyo. Njia ya pili ya miaka saba ni kipindi cha endeleo kamili.

**Niliwatoa mhanga wandugu zangu:**

Wakati wa njia yangu ya miaka 21, nina sikitiko moja tu ni kwamba sijawa bado na uwezo wa kupeleka ukweli na kushuhudia ndugu zangu. Hii ndiyo ilikuwa tena sikitiko la Yesu. Sikuweza kuongea juu ya utume wangu na ndugu zangu. Hakuna budi Wazazi wangu na kaka na dada zangu waliweza kuhisia kwamba nilikuwa mtu mmoja mkubwa, ambaye alikuwa anafanya kitu kimoja kikubwa. Sikuweza kamwe kuongea tunu ya Kanuni nao. Hii ndiyo ilikuwa kipeo changu cha maumivu. Sikuweza kuwapa upendo Wazazi wangu wala kaka na dada zangu, ingawa kimwili walikuwa karibu sana nami. Badala yake ilinipasa kupenda watu wa upande wa Kaini kuliko wa ndugu zangu. Walakini, kwa sababu hiyo, Kanisa la Umoja liliweza kuendelea mbele. Bila kupenda kwa njia hiyo, hamwezi kushinda roho ya Kaini wenu. Bila Kaini, Abeli hawezi kusimama. Bila ya kukuza watu ambao wana utiifu/utawa zaidi kwenu kuliko watoto wenu wa kimwili, hamwezi kufanya kazi ya ukombozi kwa njia ya malipizi. Ila kufanya

hivyo inamaanisha mateso makubwa.  Bila ya kuwapenda watu, mkiacha kula na kulala, hamtaweza kutawala juu yao/kuwaongoza kwa upendo.

Nilikuwa katika hali ya mambo kama hayo na nilikuwa nikijaribu kufanya msingi wa ushindi kwa njia hiyo.  Mko tofauti na mie.  Lakini, katika kipito cha pili cha miaka saba, mnaweza kuwapa wandugu, wazazi na kaka zenu vitu vyenu (tunu) vya thamani moja kwa moja, hata kuwa Masihi kwa ndugu zenu.

Wakati wa kipito cha pili cha miaka saba, mnahitaji kuwa Masihi wa kabila lenu, na mnahitaji kukamilisha ndugu zenu kile ambacho Yesu na hata mimi mwenyewe hatukuweza kufanya.  Na kwa kupata ushindi ndani ya kabila lenu, chini ya uongozi wa wazazi wenu na kaka na dada zenu, mnaweza kukamilisha kila kitu.  Mnaweza kukifanya na kiwango cha mtu peke yake, cha familia, cha kabila na cha taifa.  Na mnaweza kufungua njia ya kuelekea Dunia nzima hovyp hivyo.

Sehemu ya kuanzia pia kazi ya kipito cha pili cha miaka saba ni kufanya kile Yesu alitaka kufanya tangu miaka 2000, kueleza matakwa ya Mungu kwa Maria na Yusufu, pia kuwaacha wanashiriki kabisa kati ya maongozi yake.  Nilikuwa na nafasi ya kufanya hivyo, lakini kama ningetangulia kuwapenda ndugu zangu, hapa maongozi ya Mungu ya ukombozi yasingeendelea.

Siku zote, watu wapendwa wanatakiwa kutolewa mhanga pia wanaombwa kutwika msalaba.  Njia ya maongozi ya Mungu ilituonyesha ya kwamba yatupasa kuwatoa mhanga watoto wetu, familia yetu na kabila letu wapendwa, na kupenda kwanza familia ya Shetani, makabila ya Shetani.  Mungu anapenda na kubariki adui wake.  Yesu aliposulubiwa (aliposulubishwa) alimuomba Mungu, “Baba wasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo.”  Yesu aliweza kusema hivyo kwa sababu aliijua Roho ya Mungu.

Njia ya ukombozi haiwezi kumalizika kwa nguvu za ngumi, walakini kwa nguvu ya roho.  Ukamilisho wa malipizi unapaswa kufanywa kwa

njia hiyo. Yatupasa kujua hivyo. Yatupasa kufikiria Baraka, ambayo Yesu hakufikia. Kwa njia hiyo, ukombozi kamili na Baraka inaweza kufikika.